

**Fokasi: Misingi ya Uainishaji, Mbinu za Ung'amuzi na Mikakati ya Usimbaji katika Sentensi za Kiswahili**

**Elishafati J. Ndumiwe**  
**Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania (SAUT-Mwanza)**

ndumiweelisha@gmail.com

**Ikisiri**

Fokasi ni mojawapo ya kiambajengo cha kipragmatiki katika lugha ya Kiswahili. Uainishaji wa fokasi, mbinu za ung'amuzi wa fokasi na mikakati na usimbaji wa fokasi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Hata hivyo, katika lugha ya Kiswahili, masuala hayo hayapo bayana. Kwa hiyo, makala hii imeshughulikia misingi ya uainishaji wa fokasi, mbinu za ung'amuzi wa fokasi na mikakati ya usimbaji wa fokasi katika lugha ya Kiswahili. Data ya makala hii imekusanywa kwa kutumia mbinu ya usimulizi wa picha. Aidha, tumetumia mkabala wa kitaamuli katika uchambuzi wa data ya makala hii huku tukiongozwa na Nadharia ya Semantiki Vibandala iliyoasisiwa na Rooth (2016). Matokeo yameonesha kuwa kuna misingi minne ya uainishaji wa fokasi katika sentensi za Kiswahili. Misingi hiyo ni mazingira ya utokeaji, muundo, semantiki na lengo la mawasiliano. Aina za fokasi zilizobainika hung'amuliwa kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, usahihishaji wa taarifa au vibainishi vya fokasi. Vilevile, imebainika kuwa fokasi husimbwa katika sentensi za Kiswahili kwa kutumia mkakati wa ukasimishaji, utenguaji kushoto, unyambuaji punguzi wa vishiriki vya kitenzi, uhamishaji wa viambajengo au uwekaji wa mkazo katika tungo. Pamoja na hayo, tunapendekeza utafiti mwingine kufanyika ili kuchunguza usimbaji wa fokasi katika vipera vya fasihi simulizi kama vile nahau na hadithi.

**Dhana za Msingi:** Fokasi, usimbaji, ukasimishaji, utenguaji kushoto na ung'amuzi

## **Utangulizi**

Sentensi huundwa na viambajengo tofautitofauti vya kimuundo, kiuamilifu, kisemantiki na kipragmatiki (Jespersen, 1949). Viambajengo vya kimuundo hujumuisha darajia tatu za tungo ambazo ni kishazi, kirai na neon. Viambajengo vya kiuamilifu huonesha kazi zinazofanywa na kila kiambajengo katika sentensi. Viambajengo hivyo ni kiima, yambwa, yambiwa, chagizo na kijalizo (Hassan, 2019). Kisemantiki, sentensi huundwa na mtenda, mnufaika, mwathirika/kiathirika, mpokeaji, kitumizi, kimahali, mhisi na kithimu (Mkude, 2005 na Hassan, 2019). Kipragmatiki, sentensi huundwa na mada, maelezo na fokasi (katika mifano tumeibainisha kwa alama F). Makala hii imeshughulikia fokasi ambayo ni kiambajengo mojawapo cha kipragmatiki kinachounda sentensi. Katika lugha ya Kiswahili, eneo hili halijatafitiwa. Kwa hiyo, utafiti huu unachunguza fokasi kwa kujikita katika aina, mbinu za ung'amuzi na mikakati ya usimbaji katika lugha ya Kiswahili.

Kwa hiyo, fokasi ni taarifa mojawapo inayopatikana ndani ya sentensi. Hata hivyo, tafiti zimedhihirisha kuwa uainishaji wa fokasi hutofautiana miongoni mwa lugha za Kibantu na zisizo za Kibantu (Edenymyr, 2002; Schwarz, 2003; Kind, 2004; Van der Wal na Nyamyalo, 2016; Lafkioui, Nshemezimana na Bostoen, 2016 na Nicolle, 2016.) Vilevile, imebainika kuwa kuna aina mbalimbali za fokasi ambazo zinaweza kutokea katika lugha moja. Baadhi ya aina hizo ni fokasi tambuzi, fokasi toshelevu, fokasi linganishi, fokasi jumuishi, fokasi kamilishi, teuzi, kanushi, ongezi na badilishi.

Aina hizo hutokea katika mazingira mahususi na hutofautiana kutoka lugha moja na nyingine. Mathalani, katika lugha ya Kiganda, fokasi tambuzi

hutokea kabla ya kitenzi ilhali fokasi toshelevu hutokea baada ya kitenzi (Van der Wal na Nyamyalo, 2016). Pia, katika lugha ya Kikwaya, fokasi tambuzi hutokea kabla ya kitenzi (Nicolle, 2016). Kadhalika, Edenyumyr (2002) ameeleza kuwa, katika lugha ya Kirundi, kuna aina tofautitofauti za fokasi. Miongoni mwa aina hizo ni fokasi kamilishi, teuzi, kanushi, ongezi na badilishi. Pamoja na tafiti hizo, Krifka (2007) amefafanua aina tano za fokasi katika lugha ya Kiingereza, Kikorea na Kiitaliano. Nazo ni (i) fokasi kiambo (ii) fokasi ashirifu (iii) fokasi teuzi (iii) fokasi jumuishi na (v) fokasi linganishi.

Kutokana na tafiti mbalimbali zilizofanyika, ni wazi kwamba utokeaji wa fokasi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Hata hivyo, hakuna utafiti uliofanyika katika lugha ya Kiswahili kuonesha jinsi fokasi inavyoweza kuainishwa na mikakati ya usimbaji wake. Hivyo, lengo la makala hii ni kuchunguza usimbaji wa fokasi katika lugha ya Kiswahili kwa kujikita katika mambo matatu: misingi ya uainishaji wa fokasi, mbinu za ung'amuzi wa fokasi, na mikakati ya usimbaji wa fokasi katika sentensi za Kiswahili.

Dhana ya fokasi imeelezwa na wanasarufi tofautitofauti. Miongoni mwao ni Krifka (2007) anayeeleza kuwa fokasi ni kiambajengo kisichotabirifu kinachoweza kutokea kiubadala na kiambajengo kingine katika tungo ili kuwasilisha taarifa mpya katika sentensi. Kwa kifupi, fokasi ni taarifa mpya ambayo mtoa taarifa anahitaji imfiki mpokea taarifa.

Katika lugha ya Kiswahili, fokasi ina sifa kadhaa. Kwanza, fokasi ni kiambajengo chenye vibadala vya kimuktadha. Nafasi inayokaliwa na fokasi katika sentensi hukaliwa na kibadala kingine cha fokasi kutegemeana

na kuendana kwake kimuktadha (Krifka, 2007). Mathalani, ikiwa nomino inayorejelewa kama fokasi hutokea katika ngeli ya kwanza, kabadala chake hutokea katika ngeli ya kwanza pia.

Pili, fokasi huulizwa kwa kutumia maneno ulizi katika nafasi yake. Mara nyingi, maneno ulizi yanayotumika katika nafasi ya fokasi ni *wapi*, *nani* na *nini* (Hassan, 2019). Mifano 1 (a) na (b) inathibitisha haya.

1. (a) ki-tabu ki-li-fich-w-a **wapi?**  
Kng7-tabu Kp7-Knj-fich-tndw-Kt wapi  
'kitabu kilifichwa wapi?'
- (b) **nini** w-anafunzi wa-me-li-tekelez-a?  
nini Kng2-anafunzi Kp2-Tmlf-Ky-tekelez-Kt  
'nini wanafunzi wamelitelekeza?'

Katika mfano 1 (a), jibu linalotolewa katika nafasi ya neno ulizi (*wapi*) huwa fokasi. Katika sentensi hiyo, jibu ni mahali ambapo pamefichwa kitabu (**kabatini, uvunguni**). Vilevile, katika mfano 1 (b), jibu linalotolewa katika nafasi ya neno ulizi (*nini*) huwa fokasi. Katika sentensi hiyo, jibu ni kilichotekelezwa na wanafunzi (**agizo la mwalimu**).

Tatu, fokasi huwakilishwa na kiambishi kipatanishi cha yambwa katika kitenzi. Kiambishi yambwa katika kitenzi, hasa kitenzi kikuu, hutokea baada ya kiambishi njeo au kiambishi cha hali kwa ajili ya kupatanisha kitenzi husika na yambwa inayopaswa kujaliza kitenzi husika (Mkude, 2005). Mifano ifuatayo inadhihirisha haya.

2. (a) mw-alimu a-me-*wa*-nyim-a [w-**anafunzi**]<sub>F</sub> ruhusa.  
Kng1-alimu Kp1-Tmlf-Ky-nyim-kt Kng2-anafunzi ruhusa  
'mwalimu amewanyima wanafunzi ruhusa'  
(b) [**elimu ya nyota**,]<sub>F</sub> wa-tu ha-wa-*i*-thamini sana  
elimu ya nyota, Kng2-tu Uk-Kp2-Ky-thamini sana.  
'elimu ya nyota watu hawaithamini sana'

Katika mfano wa 2 (a), kiambishi {-wa-} kilichopachikwa katika kitenzi huiwakilisha fokasi (**wanafunzi**) katika kitenzi. Pia, katika mfano 2 (b) kiambishi {-i-} kilichopachikwa katika kitenzi huiwakilisha fokasi (**elimu ya nyota**) katika kitenzi. Katika mfano 2 (b), tunabaini kuwa kirai nomino (**elimu ya nyota**) kimetokea kabla ya kiima (watu) kutokana na mkakati wa utenguaji kushoto. Mkakati huu huondoa yambwa katika mazingira asilia, yaani mara baada ya kitenzi na kuihamishia kabla ya kitenzi au kabla ya kiima. Katika mazingira hayo, muundo msingi wa KTY hubadilika kuwa YKT. Hata hivyo, kiambishi yambwa huwa hakina ruwaza rasmi ya utokeaji wake. Mathalani, kimahali hakiwezi kupatanishwa na kiambishi yambwa (Hassan, 2019). Kwa mfano, sentensi *\*uchafu ume-ku-tapakaa sokoni*, haikubaliki katika sarufi ya Kiswahili kutokana na kuwapo kwa kiambishi cha yambwa {-ku-} katika kitenzi. Sentensi sahihi inapaswa kuwa *'uchafu umetapakaa sokoni'*. Pamoja na hayo, upo mtazamo wa wanasarufi mapokeo unaodai kuwa, kimahali kinapotokea baada ya kitenzi, huwa ni kielezi. Mtazamo huo hatukubaliani nao kwa sababu kielezi huweza kuondolewa katika tungo bila kuacha maswali ya *nani?*, *wapi?* au *nini?* lakini kimahali (nomino) kinachotokea baada ya kitenzi kinapoondolewa katika tungo huacha maswali ya *nani?*, *nini?* au *wapi?* Suala hilo linathibitishwa na Hassan (2019) anayeeleza kuwa kielezi siyo mahitaji ya lazima ya kitenzi ilhali nomino ni mahitaji ya lazima ya kitenzi.

Nne, fokasi hutokea kiasilia mara baada ya kitenzi. Mpangilio wa taarifa katika sentensi za Kiswahili (Kibantu) huruhusu taarifa mpya kutokea kiasilia mara baada ya kitenzi (Mwamzandi, 2014; Mungania na Schroeder, 2018). Kimsingi, fokasi hukamilisha taarifa kuhusu kiima (mada). Ndiyo maana hutokea kiasilia mara baada ya kitenzi ili kutoa taarifa kuhusu kiima (mada). Kimsingi, fokasi ni taarifa mpya kwa sababu haimo ndani ya uelewa wa mpokeataarifa. Mathalani, katika mfano 2 (a), fokasi “wanafunzi” imetokea mara baada ya kitenzi. Hata hivyo, upo uwezekano wa fokasi kutokea kabla ya kitenzi, yaani mazingira yasiyo asilia (Mwamzandi, 2014). Utokeaji wa fokasi katika mazingira yasiyo asilia unaweza kurejelewa katika mfano 2 (b).

Tano, fokasi ni kiambajengo cha lazima katika sentensi. Kutokana na sifa hii, uondoaji wa fokasi katika sentensi huacha maswali kwa mpokeaji wa taarifa. Hii ni kwa sababu fokasi ni taarifa ambayo msemaji/mwandishi anakusudia imfikie msikilizaji/msomaji. Aidha, fokasi inapoondolewa katika sentensi huacha swali la wapi, nini, nani au lipi. Kwa mfano, katika sentensi: “*mama anachoja maji*” tukiondoa neno “*maji*” na sentensi kuwa: *mama anachota lazima mpokea taarifa ajiulize nini kinachotwa?*

***Mbinu za ung’amuzi wa fokasi katika lugha za Kibantu***

Mbinu za ung’amuzi wa fokasi humsaidia mwanasarufi kutambua kuwa kiambajengo cha sentensi kimetokea kama fokasi au la (Krifka (2007; Van der Wal, 2016). Vilevile, mbinu hizi humsaidia mwanasarufi kubainisha fokasi miongoni mwa vijenzi vingine vya sentensi katika mkabala wa kipragmatiki. Baadhi ya wanasarufi wamependekeza mbinu tofautitofauti za ung’amuzi wa fokasi katika lugha. Miongoni mwao ni Van der Wal (2016) aliyependekeza mbinu saba za ung’amuzi wa fokasi kwa kutumia mifano

kutoka lugha ya Kiingereza, Kihausa, na Kiganda. Mbinu hizo ni ubunifu wa kimuktadha, vikumushi vya nomino, maswali na majibu, vibainishi vya fokasi, usahihishaji wa taarifa, muktadha, na vimanilizi.

Nao Van der Wal na Nyamyalo (2016) wameonesha kuwa fokasi tambuzi inayotokea kabla ya kitenzi katika lugha ya Kiganda hung'amuliwa kwa kutumia mbinu nne ambazo ni maswali na majibu, vikumushi vya nomino, vibainishi vya fokasi, na usahihishaji wa taarifa. Aidha, fokasi ya pekee inayotokea baada ya kitenzi hung'amuliwa kwa kutumia mbinu tano ambazo ni maswali ya vidadala, usahihishaji wa taarifa, vikumushi vya nomino, vibainishi vya fokasi, na tafsiri funge ya maswali kuhusu mhusika. Pamoja na hao, Van der Wal (2021) ameeleza matumizi ya nahau katika ung'amuzi wa fokasi katika lugha tofautitofauti za Kibantu. Miongoni mwa lugha alizoshughulikia ni Kiganda, Kimakua, Kibukusu, Kirundi, Kimatengo, Kiitharaka, Kinyakyusa na Kizulu. Katika andiko hilo, anaonesha kuwa, vijenzi vya nahau vinapotungiwa sentensi, maana ya msingi ya nahau huweza kubakia au kutoweka. Ubakiaji wa maana ya nahau huonesha kuwa mkakati uliotumika katika kuunda sentensi hausimbi fokasi. Lakini, maana ya kinahau inapoondoka, huonesha kuwa mkakati huo hutumika katika usimbaji wa fokasi katika lugha husika.

Kutokana na ufafanuzi wa Krifka (2007), Van der Wal (2016), Van der Wal na Nyamyalo (2016), na Van der Wal (2021) imedhihirika kuwa fokasi katika lugha walizozichunguza hung'amuliwa kwa kutumia mbinu tofautitofauti. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili si miongoni mwa lugha zilizochunguzwa. Kutokana na hilo, makala hii imehakiki kama mbinu hizo zinaweza kutumika kung'amua usimbaji wa fokasi katika sentensi za Kiswahili. Kwa hiyo, mbinu tatu zimetumika katika makala hii kung'amua

fokasi katika sentensi za Kiswahili. Mbinu hizo ni jozi ya maswali na majibu, vibainishi vya fokasi na usahihishaji wa taarifa. Mbinu hizi zimetumika kwa sababu ndizo huendana na data ya lugha ya Kiswahili.

### ***Mikakati ya usimbaji wa fokasi***

Mikakati ya usimbaji wa fokasi ni taratibu za kiisimu (kisarufi) za upakiaji wa taarifa mpya katika sentensi (Krifka, 2007 na Van der Wal na Nyamyalo, 2016). Mikakati ya usimbaji wa fokasi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Wanaisimu mbalimbali wamebaini kuwa usimbaji wa fokasi katika lugha za Kibantu hutumia mikakati ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia au kimofosintaksia (Yonenda, 2011 na Van der Wal na Nyamyalo, 2016). Mikakati ya kisintaksia hujumuisha ukasimishaji, utenguaji kushoto, upinduzi wa vishiriki na uhamishaji mwanzoni (Edelsten na wenzake, 2013; Lafkiou na wenzake, 2016). Mikakati ya kifonolojia hujumuisha uwekaji mkazo, uwekaji wa pumziko fupi na uhamishaji toni (Landman na Ranero, 2018). Mikakati ya kimofosintaksia hujumuisha unyambujaji punguzi na ongezi wa vishiriki vya kitenzi (Mwamzandi, 2014). Vilevile, mikakati ya kimofolojia hujumuisha uondoaji wa kiambishi tangulizi katika nomino na uambishaji wa kibainishi (ne-/n) kabla ya kitenzi (Schwarz, 2003 na Landman na Ranero, 2018)

### **Methodolojia**

Data ya makala hii imekusanywa kwa kutumia mbinu ya usimulizi wa picha. Mtafiti alitumia mbinu ya usimulizi wa picha kwa sababu utokeaji wa fokasi hutegemea muktadha wa mazungumzo kati ya watu wawili au zaidi. Mtafiti alitengeneza picha zenye maudhui tofautitofauti yanayohusu binadamu, wanyama, ndege na vitu vingine. Aliwapatia watoa taarifa watunge sentensi kuhusu picha hizo kwa kuzingatia maudhui yaliyomo



kwenye picha husika. Wazungumzaji watatu wa lugha ya Kiswahili kutoka kata ya Luchelele iliyopo wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza waliteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha kujua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili. Eneo la utafiti lilitolewa kinasibu kuwakilisha maeneo mengine ambayo wazungumzaji wa Kiswahili wanaojua kusoma na kuandika wanaweza kupatikana.

Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli huku tukiongozwa na Nadharia ya Vibandala vya Kisemantiki iliyopendekezwa na Rooth (2016) ili kushughulikia kategoria za muundo taarifa katika lugha ya Kiingereza, Kijerumani, Kikorea, na Kijapani. Nadharia hii inaelezwa kuwa, fokasi huchochea kutokea vibadala vya kimuktadha katika kilongo. Mazingira ambamo fokasi hutokea, kiambajengo kingine chenye hadhi ya namna hiyo huweza kutokea. Kwa kutumia nadharia hii, tumebaini aina tofautitofauti za fokasi katika lugha ya Kiswahili kwa kujikita katika misingi ya uainishaji. Vilevile, tumeweza kuonesha mbinu za ung'amuzi na mikakati ya kisarufi inayosimba fokasi husika.

### **Matokeo ya Utafiti**

Katika makala hii, imebainika kuwa kuna misingi minne ya uainishaji wa fokasi. Misingi hiyo ni muundo, mazingira ya utokeaji, semantiki, na lengo la mawasiliano. Ubainishaji wa aina za fokasi katika lugha ya Kiswahili umezingatia dhana ya vibadala kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Vibandala vya Kisemantiki ya Rooth (2016). Aidha, kila aina iliyobainika hung'amuliwa kwa kutumia mbinu mwafaka. Vilevile, fokasi hiyo husimbwa kwa kutumia mkakati mwafaka wa kisarufi.

### **Msingi wa kimuundo, mbinu za ung'amuzi na mikakati ya usimbaji**

Msingi huu huzingatia muundo wa kiambajengo kinachorejelewa kama fokasi katika sentensi husika. Kwa kigezo hiki, fokasi inaweza kuwa neno/kirai, kiarifu, au sentensi nzima. Kwa hiyo, kwa kuzingatia msingi wa kimuundo, imebainika kuwa kuna aina tatu za fokasi ambazo ni kishiriki, kiarifu, na sentensi.

#### ***Fokasi kishiriki***

Fokasi kishiriki ni taarifa mpya inayobebwa na kirai nomino, kirai kihusishi, au kirai kielezi kinachotokea kama kiambajengo kimoja. Aina hii ya fokasi hutokea mara baada ya kitenzi katika mpangilio wa kiima-kitenzi-yambwa (KTY). Kutokana na maelezo haya, fokasi kishiriki hutokea ikiwa sentensi ina kitenzi elekezi chenye uwezo wa kungoeka yambwa moja au zaidi. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya.

3. (a) Watoto walisafiri [*kwa gari la shule*]<sub>F</sub>
  - (b) Wanafunzi wanacheza [*mpira wa wavu*]<sub>F</sub>
  - (c) Mjamzito hutembea [*polepole*]<sub>F</sub>
  - (d) Mwalimu anampiga [*Ashura*]<sub>F</sub> fimbo kichwani.
- Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Viambajengo vilivyokolezwa katika mfano wa 3 (a) - (d) ndivyo hubeba fokasi. Katika mfano wa 3 (b), na (d) kirai nomino katika sentensi ndicho hubeba fokasi katika sentensi hizo. Aidha, katika mfano wa 3 (a) kirai kihusishi ndicho kimebeba fokasi. Vilevile, katika mfano wa 3 (c) kirai kielezi ndicho kimebeba taarifa mpya katika sentensi. Sambamba na hayo, fokasi imetokea katika mazingira asilia, yaani mara baada ya kitenzi. Hata hivyo, kuna uwezekano wa fokasi kishiriki katika lugha ya Kiswahili kutokea katika mazingira yasiyo asilia. Mara nyingi, mazingira hayo huwa ni kabla ya kitenzi au kabla ya kiima. Mifano ifuatayo inadhihirisha

utokeaji wa fokasi katika mazingira yasiyo asilia, yaani kabla ya kitenzi au kabla ya kiima.

4. (a) [**Kikombe cha kijani**]<sub>F</sub>, alikivunja mtoto.  
(b) [**Kwa maringo**]<sub>F</sub>, kinyonga hutembea.  
(c) [**Polepole**]<sub>F</sub>, mama alimuachia mtoto.  
(d) [**Ashura**]<sub>F</sub>, ndiye aliyempiga mtoto.  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Viambajengo vilivyokolezwa katika mfano wa 4 (a) - (d) ndivyo vimebeba fokasi. Aidha, mbinu ya maswali na majibu hutumika katika ung'amuzi wa fokasi kishiriki katika lugha ya Kiswahili. Kiambajego ulizi katika sentensi ya swali hutokea kiubadala na kiambajengo cha jibu katika sentensi ya majibu. Mathalani, fokasi zilizopo kwenye tungo 3 (a) - (d) huweza kuulizwa kwa namna tofautitofauti kama ye fokasi tunaweza kuweka viulizi kama inavyoonekana katika mfano 5 (a) - (d).

5. (a) Watoto walisafiri *kivipi*?  
(b) Wanafunzi wanacheza *nini*?  
(c) Mjamzito hutembea *kivipi*?  
(d) Mwalimu anampiga *nani* fimbo kichwani?  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Mazingira yenye viambajengo ulizi ndipo fokasi kishiriki huweza kutokea katika mfano 5 (a) - (d). Vilevile, katika mfano wa 4 (a) - (b) viambajengo ulizi huweza kutokea kiubadala na fokasi kishiriki kama inavyodhihirika katika 6 (a) - (d).

6. (a) *Nini* alikivunja mtoto?  
(b) *Ni kwa vipi* kinyonga hutembea?  
(c) *Ni kwa vipi* mama alimuachia mtoto?  
(d) *Ni nani* aliyempiga mtoto?  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Kwa hiyo, maswali na majibu ni mojawapo ya mbinu ya ung'amuzi wa fokasi kishiriki katika sentensi za Kiswahili. Kiambajengo ulizi katika sentensi ya swali hujibiwa na fokasi katika sentensi ya jibu.

Pamoja na hayo, fokasi kishiriki kama ilivyoelezwa katika kipengele hiki husimbwa kwa kutumia mikakati kadhaa ya kisarufi. Mathalani, katika mfano wa 3 (a) - (d) fokasi kishiriki imetokea katika mazingira asilia, yaani mara baada ya kitenzi. Katika mazingira haya fokasi husimbwa kwa kutumia mkakati wa uwekaji mkazo katika tungo. Aidha, katika 4 (a) mkakati uliohusika kusimba fokasi kabla ya kitenzi ni utenguaji kushoto. Vilevile, katika 4 (b) na (c) mkakati uliohusika ni uhamishaji wa viambajengo. Pia, katika 4 (d) mkakati uliohusika ni ukasimishaji.

### ***Fokasi kiarifu***

Fokasi kiarifu ni taarifa mpya inayobebwa na kitenzi sielekezi. Kitenzi hiki huwa hakihitaji yambwa halisi au yambiwa. Sentensi yenye kitenzi sielekezi huwa na kiima tu. Mara nyingi, kitenzi kinaweza kuwa sielekezi kwa asili yake au baada ya unyambuaji punguzi wa vishiriki vya kitenzi kama vile utendano au utendeka (Ndumiwe, 2020). Fokasi kiarifu katika sentensi za Kiswahili hung'amuliwa kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu. Mara nyingi, swali huulizwa kuhusu nini kinafanywa na kiima. Jibu linalotokea hueleza tendo linalofanywa na kiima. Kwa hiyo, jibu lake ndilo hutokea kama fokasi kiarifu katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano:

7. (a) Mbwa wa kizungu *wanafanya nini?*  
(b) Wazee wenye mvi *wanafanyaje?*  
(c) Kikombe *kimekuwaje?*  
(d) Ali na Juma *wanafanya nini?*  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Majibu ya maswali katika mfano wa 7 (a) - (d) hupatikana katika 8 (a)-(d) kwa kuonyesha tendo linalofanywa na kiima. Tendo hilo ndilo husimbwa kama fokasi kiarifu katika sentensi za Kiswahili. Mifano ifuatayo inaonesha fokasi kiarifu katika Kiswahili.

8. (a) Mbwa wa kizungu [wanabweka]<sub>F</sub>.  
(b) Wazee wenye mvi [wanacheka].  
(c) Kikombe [kimevunjika kidogo]<sub>F</sub>.  
(d) Ali na Juma [wanapigana sana]<sub>F</sub>.  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Viambajengo vilivyokolezwa katika mfano wa 8 (a) - (d) ndivyo vimebeba fokasi inayopaswa kumfikia mpokeataarifa. Katika mfano wa 8 (a) na (b), fokasi imesimbwa kiasilia katika vitenzi sielekezi 'bweka' na 'cheka' mtawalia. Katika mfano wa 8 (c) na (d), fokasi imesimbwa na vitenzi sielekezi baada ya unyambuaji punguzi wa vishiriki vya kitenzi, yaani utendeka na utendano mtawalia. Ieleweke kuwa kitenzi 'vunja' na 'piga' ni elekezi, yaani huhitaji mtenda na kiathirika/mwathirika, lakini baada ya kunyambuliwa kwa kutumia viambishi vya kauli ya utendeka {-ik-} na utendano {-an-} vimebadilika na kuwa vitenzi sielekezi. Kwa maana hiyo, unyambuaji wa utendeka na utendano umevibadili kutoka elekezi kuwa sielekezi.

Kimsingi, fokasi kiarifu katika lugha ya Kiswahili, hutokea mara baada ya kiima. Kwa maelezo hayo, fokasi kiarifu katika vitenzi sielekezi asilia

katika mfano wa 8 (a) na (b) husimbwa kwa kutumia mkakati wa uwekaji mkazo katika tungo. Aidha, fokasi kiarifu katika vitenzi sielekezi baada ya unyambujaji tendeka na tendano katika mfano wa 8 (c) na (d) husimbwa kwa kutumia mkakati wa unyambujaji punguzi wa vishiriki vya kitenzi.

### ***Fokasi sentensi***

Fokasi sentensi ni fokasi inayohusu sentensi nzima kama taarifa mpya, yaani kiima na kiarifu chake hutokea kama taarifa mpya katika usemi (Lambrecht na Polinsky, 1997). Lengo lake ni kuarifu jambo fulani, hasa baada ya kuulizwa kuhusu jambo hilo (Hassan, 2019). Kwa maana hiyo, jibu la swali litakuwa na sentensi nzima ambayo husimbwa kama fokasi. Mfano wa 9 unadhihirisha haya.

9. (i) **A:** nini kimetokea?  
**B:** [Kikombe kimevunjika chote]<sub>F</sub>.
- (ii) **A:** nini kimefanyika?  
**B:** [mbwa wa kizungu amebweka sana]<sub>F</sub>.  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Majibu katikamfano wa 9 (i) (B) na (ii) (B) ndiyo hubeba fokasi inayokusudiwa kumfikia mpokea taarifa. Tofauti na aina nyingine, fokasi hii hutokea kama sentensi nzima kwa sababu taarifa nzima inayotolewa na mtoa taarifa huwa ni mpya kwa mpokea taarifa. Fokasi ya aina hii hung'amuliwa kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu kama inavyojidhihirisha katika mfano wa 9 (i) na (ii).

### **Msingi wa mazingira ya utokeaji, mbinu za ung'amuzi na mikakati ya usimbaji**

Fokasi hutokea katika mazingira mahususi kutegemeana na muundo wa tungo husika (Mungania na Schroeder, 2018). Aidha, Van der Wal na Nyamyalo (2016) wanaeleza kuwa katika lugha za Kibantu fokasi hutokea

katika mazingira asilia au yasiyo asilia. Kwa kuzingatia kigezo hiki, kuna aina mbili za fokasi ambazo ni fokasi dhahiri na iso-dhahiri.

### ***Fokasi dhahiri***

Fokasi dhahiri hutokea katika mazingira yasiyo asilia, yaani kabla ya kitenzi. Fokasi hii hutokana na upanguaji wa muundo wa tungo unaosababisha fokasi kutokea nje ya mipaka yake. Mara nyingi, mkakati wa utenguaji kushoto na uhamishaji wa viambajengo ndiyo husimba fokasi katika mazingira yasiyo asilia. Kwa mfano:

10. (a) **[Kikombe cha kijani]<sub>F</sub>**, alikivunja mtoto.  
(b) **[Kwa maringo]<sub>F</sub>**, kinyonga hutembea.  
(c) **[Ashura]<sub>F</sub>**, ndiye aliyempiga mtoto.  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Katika mfano wa 10 (a) - (c) inabainika kuwa fokasi dhahiri inatokea mwanzoni mwa sentensi huku ikifuatiwa na pumziko fupi kabla ya kuendelea na vijenzi vingine. Aina hii ya fokasi imetokea katika mazingira yasiyo asilia baada ya upanguaji wa viambajengo kufanyika.

Katika lugha ya Kiswahili, fokasi dhahiri hung'amuliwa kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu. Kiambajengo ulizi kinawekwa katika nafasi ya fokasi na jibu linalotokea katika nafasi hiyo huwa ndiyo fokasi. Mathalani, katika mfano wa 10 (a) - (c), sehemu yenye fokasi dhahiri tunaweka maneno ulizi katika sentensi swalifu kama inavyoonekana katika mfano wa 11 (a) - (c).

11. (a) **Nini**, alikivunja mtoto?  
(b) **Kivipi**, kinyonga hutembea?  
(c) **Nani** aliyempiga mtoto?  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Katika mfano wa 11 (a) - (c), sehemu zenye viambajengo ulizi hukaliwa na fokasi dhahiri katika sentensi arifu. Kwa hiyo, mbinu ya swali na jibu lake hutusaidia kung'amua fokasi katika sentensi za Kiswahili.

Pamoja na hayo, mkakati unaohusika katika usimbaji wa fokasi dhahiri katika mfano wa 10 (a) na (c) ni mkakati wa utenguaji kushoto. Sanjari na hayo, usimbaji wa fokasi kwa kutumia mkakati huu hubadilisha muundo msingi wa lugha ya Kiswahili kutoka KTY kuwa YTK. Aidha, katika mfano wa 10 (b) mkakati wa usimbaji wa fokasi uliotumika ni uhamishaji wa fokasi.

### ***Fokasi iso-dhahiri***

Fokasi iso-dhahiri hutokea katika mazingira asilia, yaani nafasi ya yambwa. Fokasi hii hutokea katika tungo yenye muundo wa KTY. Katika muundo huu, fokasi husimbwa katika kiambajengo kinachotokea mara baada ya kitenzi.

12. (a) Mbuzi anakula [**majani ya mahindi**]<sub>F</sub>  
(b) Wanafunzi wanacheza [**mpira wa wavu**]<sub>F</sub>  
(c) Watoto wanavuta [**kamba**]<sub>F</sub>  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Katika mfano wa 12 (a) - (c), tunaona kuwa fokasi zimetokea mara baada ya kitenzi. Mazingira haya ndiyo hurejelewa kama utokeaji kiasilia katika lugha za Kibantu. Ung'amuzi wa aina hii ya fokasi unaweza kutumia jozi ya maswali na majibu ambapo maswali huulizwa katika nafasi ya fokasi. Mathalani, katika mfano wa 12 (a) - (c), viambajengo ulizi huwekwa katika nafasi ya fokasi kama inavyoonekana katika mfano wa 13 (a) - (c).



13. (a) Mbuji anakula *nini*?  
(b) Wanafunzi wanacheza *nini*?  
(c) Watoto wanavuta *nini*?  
Chanzo: Data za Utafiti (2022)

Kutokana na mfano wa 13 (a) - (c), maneno yaliyokolezwa ni viulizi ambavyo hutokea kiabadala na fokasi katika tungo hizo. Kwa hiyo, maswali na majibu ni mbinu mojawapo ya ung'amuzi wa fokasi katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, fokasi iso-dhahiri inayotokea katika mazingira asilia, yaani mara baada ya kitenzi husimbwa kwa kutumia mkakati wa uwekaji mkazo katika tungo. Katika lugha ya Kiswahili, mkazo ambao hutokea katika neno la mwisho katika tungo ndiyo husimba fokasi iso-dhahiri katika sentensi za Kiswahili.

**Msingi wa kisemantiki, mbinu za ung'amuzi na mikakati ya usimbaji**  
Msingi wa kisemantiki huzingatia dhana inayobebwa na kiambajengo kinachorejelewa kama fokasi. Kwa kawaida, viambajengo vilivyopo katika sentensi hubeba taarifa mbalimbali kutegemeana na dhamira ya msemaji/mwandishi (Zimmermann, 2008). Kwa kuzingatia msingi huu, kuna aina tatu za fokasi katika lugha ya Kiswahili. Nazo ni fokasi kinzani, tambuzi, na toshelevu.

### ***Fokasi kinzani***

Fokasi kinzani ni kiambajengo kinachobeba taarifa mpya kutoka kwa mpokea taarifa inayokinzana na matarajio ya mtoa taarifa (Krifka, 2007 na Zimmermann, 2008). Mara nyingi, hujitokeza katika mazungumzo yanayohusisha pande mbili. Pande hizo zinaweza kuhusisha maswali na

majibu au taarifa inayohitaji mwitiko wa mpokea taarifa. Katika mazingira hayo, yale majibu au mwitiko wa mpokea taarifa hukinzana na matarajio ya mtoa taarifa. Kwa mfano:

14. A: Wanafunzi wanacheza mpira  
B: Hapana, wanacheza [**mchezo wa kuvuta kamba**]<sub>F</sub>.
15. A: Unaosha sufuria?  
B: Hapana, ninaosha [**ndoo**]<sub>F</sub>.  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Jibu katika mfano wa 14 (B) linatofautiana na matarajio ya muulizaji katika mfano wa 15 (A), ambapo alidhani kuwa mjibuji anaosha sufuria kumbe anaosha ndoo. Vilevile, katika mfano wa 14 (B), mpokea taarifa anatoa mwitikio unaotofautiana na taarifa aliyoitoa mtoa taarifa. Kwa hiyo, mwitikio na majibu katika mazingira haya hutokea kama fokasi kinzani katika lugha ya Kiswahili. Ung'amuzi wa aina hii ya fokasi hutumia mbinu ya usahihishaji wa taarifa. Mwitiko wa msikilizaji husahihisha taarifa iliyotolewa na mzungumzaji kama inavyoonekana katika mfano wa 14 (B) na 15 (B).

Aidha, fokasi kinzani inayotokea mara baada ya kitenzi husimbwa kwa kutumia mkakati wa uwekaji wa mkazo katika tungo. Katika lugha ya Kiswahili, mkazo ambao hutokea katika neno la mwisho katika tungo ndiyo husimba fokasi kinzani kama inavyoonekana katika mfano wa 14 (B) na 15 (B).

### ***Fokasi tambuzi***

Fokasi tambuzi ni kiambajengo kinachotokana na udhanalizo wa tendo lililofanyika kujikita katika kirejelewa fulani miongoni mwa virejelewa

vingine (Kiss, 1998 na Van der Wal na Nyamyalo, 2016). Ifuatayo ni aadhi ya mifano ya fokasi tambuzi katika lugha ya Kiswahili:

16. (a) Ni [**babu**]<sub>F</sub> anayechunga mbuzi.  
(b) [**Babu**]<sub>F</sub> ndiye anayechunga mbuzi.  
(c) Anayechunga mbuzi ni [**babu**]<sub>F</sub>.  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Katika mfano 16 wa (a) - (c), kuna udhanio kuwa mbuzi anachungwa na mtu fulani. Aidha, anayetambuliwa kuwachunga mbuzi hao ni babu. Yamkini, wapo watu wengi, lakini anayetambuliwa miongoni mwa watu hao ni babu. Kwa hiyo, kiambajengo ‘*babu*’ katika mfano wa 16 (a) - (c) huchukuliwa kama fokasi tambuzi. Ung’amuzi wa aina hii ya fokasi hutumia mbinu ya maswali na majibu. Mfano wa 16 (a) - (c) ni majibu ya swali la “*nani anayechunga mbuzi?*” Jibu lake (babu) limetokea katika mazingira tofautitofauti ya sentensi kutegemeana na dhamira ya msemaji.

Aina hii ya fokasi imesimbwa kwa kutumia mkakati wa ukasimishaji. Katika mkakati huu, sentensi sahili hugawanywa katika vishazi viwili kwa lengo la kuonesha taarifa mpya katika sentensi. Sambamba na matokeo haya, Lafkioui na wenzake (2018) wanaonesha kuwa fokasi tambuzi katika lugha ya Kirundi hutokea katika sentensi kasimiwa.

### ***Fokasi toshelevu***

Fokasi toshelevu ni kiambajengo kinachochochea uondoaji wa vibadala vingine na kubakia peke yake katika tungo (Van der Wal, 2014, Van der Wal na Nyamyalo, 2016). Kiambajengo hiki hutokea mara baada ya kitenzi katika lugha zenye muundo msingi wa KTY. Utokeaji wa fokasi toshelevu hauambatani na udhanalizo wowote. Pia, hakuna uwezekano wa kiambajengo kingine kutokea katika mazingira hayo. Wakati mwingine,

fokasi toshelevu huambatana na kibainishi cha pekee “tu”. Mifano ifuatayo inadhahirisha haya:

17. (a) Wanafunzi wa kike wanacheza [**mpira wa wavu**]<sub>F</sub>.  
(b) Mwalimu anaandika [**ubaoni**]<sub>F</sub>.  
(c) Mteja amenunua [**maembe**]<sub>F</sub> tu.  
(d) Mbuzi anakula [**mahindi**]<sub>F</sub> tu  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Maneno yaliyokolezwa katika wa 17 (a) - (d), yanawakilisha fokasi toshelevu. Matalani, katika mfano wa 17 (a), fokasi “mpira wa wavu” imeondoa vidabala vingine kama vile mpira wa pete, mpira wa miguu, mpira wa mikono na mpira wa kikapu. Kwa hiyo, fokasi inayotokea katika mazingira hayo huitwa fokasi toshelevu. Vilevile, katika mfano wa 17 (d), kibainishi cha fokasi “tu” kimeondoa vibadala vingine kama vile uwele, mtama, majani, maharage na kunde. Uondoaji wa vibadala vingine umesababisha mahindi kuwa kibandala cha pekee. Fokasi toshelevu huweza kung’amuliwa kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu. Mazingira ambayo fokasi toshelevu hutokea tunaweka viambajengo ulizi. Majibu yanayotokea katika mazingira hayo ndiyo hurejelewa kama fokasi toshelevu. Kwa hiyo, katika mfano wa 17 (a) - (d), tunaweza kuweka viambajengo ulizi kama inavyoonekana katika mfano wa 18 (a) - (d).

18. (a) Wanafunzi wa kike wanacheza **nini**?  
(b) Mwalimu anaandika **wapi**?  
(c) Mteja amenunua **nini**?  
(d) Mbuzi anakula **nini**?  
**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Vimbajengo vilivyokolezwa katika mfano wa 18 (a) - (d) ni viulizi ambavyo nafasi yake huweza kukaliwa na fokasi toshelevu katika tungo

husika. Kwa hiyo, mbinu ya maswali na majibu hung'amua utokeaji wa fokasi toshelevu katika tungo za Kiswahili.

Mazingira ya utokeaji wa fokasi toshelevu katika mfano wa 17 (a) - (d), yaani mara baada ya kitenzi huonesha kuwa fokasi aina hii husimbwa na mkazo ambao katika lugha ya Kiswahili hutokea katika silabi ya pili ya neno la mwisho la tungo.

### **Msingi wa lengo la mawasiliano, mbinu za ung'amuzi na mikakati ya usimbaji**

Lengo la mawasiliano huangalia dhima ya kiambajengo kinachorejelewa kama fokasi katika mawasiliano (Dik, 1997a). Kwa mujibu wa Dik (1997b), lengo la mawasiliano huwa ni kujaza taarifa katika ombwe au kuwasilisha taarifa tofauti na iliyotolewa. Aina ya fokasi inayojaza ombwe hutokana na uulizaji wa swali/maswali (Edenmyr, 2002). Hii ina maana kwamba, swali linapoulizwa, huwa na taarifa inayohitaji kukamilishwa.

Aidha, Edenmyr (2002) anaeleza kuwa aina nyinginezo za fokasi kwa kigezo hiki huwa na lengo la kuwasilisha taarifa tofauti kati ya fokasi na vibadala vingine ambavyo vinaweza kuwa vimedhanalizwa. Kwa maelezo hayo, tumebaini aina tofautitofauti za fokasi katika lugha ya Kiswahili kwa kigezo cha lengo la mawasiliano. Nazo ni fokasi kamilishi, teuzi, kanushi, ongezi na badilishi.

### ***Fokasi kamilishi***

Fokasi kamilishi ni fokasi yenye lengo la kujaza taarifa katika ombwe lililoachwa na swali. Aina hii hutokea sambamba na uulizaji wa swali/maswali. Uulizaji wa taarifa humaanisha kuwa kuna taarifa inayokosekana, yaani haimo katika maarifa ya mtoa taarifa. Kwa hiyo, jibu

linalotolewa hujaza ombwe la taarifa iliyokuwa inakosekana. Katika mazingira haya, ndipo jibu la swali huwa fokasi kamilishi. Kwa mfano:

19. (i) **A:** Mtoto amevunja nini?  
**B:** Ni [**Kikombe**]<sub>F</sub> kilichovunjwa na mtoto.
- (ii) **A:** Kikombe kimekuwaje?  
**B:** Kikombe [**kimevunjika**]<sub>F</sub>.
- (iii) **A:** Nini kimetokea?

Katika mfano wa 19 (i) - (iii), maneno yaliyokolezwa ni fokasi kamilishi zinazokamilisha ombwe la taarifa iliyokosekana katika taarifa ya muuliza swali. Fokasi kamilishi hujaza taarifa hiyo kwa muuliza swali. Kwa hiyo, mbinu ya maswali na majibu ndiyo husaidia katika ung'amuzi wa fokasi kamilishi katika tungo za Kiswahili kama inavyoonekana katika mfano wa 19 (i) - (ii) katika maswali na majibu yake.

Fokasi kamilishi husimbwa na mikakati tofautitofauti ya kisarufi. Mathalani, katika mfano wa 19 (i) B, fokasi kamilishi (kikombe) imesimbwa kwa kutumia mkakati wa ukasimishaji. Vilevile, katika mfano wa 19 (ii), fokasi kamilishi (kimevunjika) imesimbwa kwa kutumia mkakati wa unyambuzi punguzi wa vishiriki vya kitenzi. Pia, katika mfano wa 19 (iii) B, fokasi kamilishi imesimbwa kwa kutumia mkakati wa uwekaji mkazo katika silabi ya pili kutoka mwisho ya neno la mwisho katika tungo.

### ***Fokasi teuzi***

Fokasi teuzi ni kiambajengo kinachoteuliwa miongoni mwa viambajengo kadhaa vinavyoorodheshwa na mzungumzaji. Msikilizaji huteua mojawapo katika vile vilivyoorodheshwa. Kwa hiyo, fokasi huteuliwa miongoni mwa orodha iliyowekwa na mzungumzaji siyo nje ya orodha hiyo. Kwa mfano:

20. **A:** Mtoto alikula mkate, kokoto, chungwa au andazi?  
**B:** [chungwa] <sub>F</sub> ndilo lililoliwa na mtoto.  
Chanzo: Data ya Uwandani (2022)

Katika mfano wa 20 (A), kuna orodha ya vitu vingi ambavyo vinasadikika kuliwa na mtoto. Aidha, msikilizaji ameteua kimojawapo tu (chungwa) katika orodha hiyo. Kwa hiyo, kiambajengo kilichoteuliwa ndicho hurejelewa kama fokasi teuzi. Ung'amuzi wa fokasi ya aina hii hutumia mbinu ya maswali na majibu kama inavyoonekana katika mfano wa 20 A (swali) na B (jibu lake). Aidha, fokasi teuzi katika mfano wa 20 (B) husimbwa kwa kutumia mkakati wa ukasimishaji.

### ***Fokasi kanushi***

Fokasi kanushi ni fokasi yenye lengo la kukanusha taarifa iliyotolewa na mzungumzaji/mwandishi. Katika aina hii, mzungumzaji/mwandishi hudhani kuwa taarifa anayoitoa ndiyo sahihi lakini msikilizaji/msomaji huikataa taarifa hiyo bila ya kutoa taarifa ambayo yeye anadhani ni sahihi. Mifano ifuatayo inadhihirisha fokasi kanushi katika lugha ya Kiswahili.

21. (i) **A:** Bibi amenunua machungwa  
**B:** Hapana, hakununua [machungwa] <sub>F</sub>.  
(ii) **A:** Babu anachunga mbuzi  
**B:** Hapana, hachungi [mbuzi] <sub>F</sub>.  
Chanzo: Data ya Uwandani (2022)

Mfano wa 21 (i) B na (ii) B, unawakilisha fokasi kanushi ndani yake. Katika mifano hiyo, taarifa iliyotolewa na mzungumzaji katika 21 (i) A na (ii) A inakanushwa na msikilizaji bila kutoa nyingine ambayo huwakilisha kile kinachotendwa na mtenda. Ung'amuzi wa aina hii ya fokasi hutumia mbinu ya usahihishaji wa taarifa. Mwitiko wa msikilizaji husahihisha

taarifa iliyotolewa na mzungumzaji kama inavyoonekana katika mfano wa 21 (i) B na (ii) (B).

Aidha, fokasi kanushi inayotokea mara baada ya kitenzi husimbwa kwa kutumia mkakati wa uwekaji wa mkazo. Katika lugha ya Kiswahili, mkazo ambao hutokea katika neno la mwisho katika tungo ndiyo husimba fokasi kanushi katika sentensi za Kiswahili kama inavyoonekana katika mfano wa 21 (i) B na (ii) (B).

### ***Fokasi ongezi***

Fokasi ongezi ni kiambajengo kinachoongeza taarifa nyingine katika taarifa iliyokuwapo awali. Mzungumzaji hutoa taarifa ambayo haijakamilika, lakini msikilizaji wake huiongezea taarifa ile kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile matumizi ya maneno ongezi (pia au na). Kwa maana hiyo, tunatarajia fokasi ongezi iwe kiambajengo kipya tofauti na vile/kile kilichotolewa na mzungumzaji. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya.

22. (i) **A:** Mtoto amekula ndizi  
**B:** Ndiyo, amekula na [**machungwa**]<sub>F</sub> pia.
- (ii) **A:** Babu anachunga mbuzi  
**B:** Babu hachungi mbuzi tu, pia anachunga [**kondoo**]<sub>F</sub> na [**ng'ombe**]<sub>F</sub>  
Chanzo: Data ya Uwandani (2022)

Katika mfano wa 22 (i) B na (ii) B, vipashio vilivyokolezwa vimeongezwa na msikilizaji baada ya mzungumzaji katika mfano wa 22 (i) A na (ii) A kutokutoa taarifa hiyo. Kwa hiyo, vipashio hivyo, vimetokea kama fokasi ongezi katika tungo tajwa. Fokasi ya aina hii hung'amuliwa kwa kutumia mbinu ya vibainishi vya fokasi. Vibainishi vya fokasi huonesha taarifa iliyoongezwa. Mathalani, katika mfano wa 22 (i) B na (ii) B, viambajengo 'pia' na 'na' hutumika kung'amua fokasi ongezi katika tungo hizo. Aidha,



fokasi ongezi husimbwa kwa kutumia mkakati wa uwekaji wa mkazo katika tungo.

***Fokasi badilishi***

Fokasi badilishi ni aina ya fokasi yenye kuondoa taarifa ya mzungumzaji na kuweka taarifa mpya tofauti na ile iliyokuwapo. Katika aina hii, mwitiko wa msikilizaji huanza kwanza kukanusha taarifa ya mzungumzaji, kisha kutoa taarifa mbadala ya ile iliyowasilishwa. Fokasi badilishi inaweza kubebwa na kirai nomino kinachotokea baada ya kitenzi au kitenzi kilichopo katika mwitiko wa msikilizaji. Kwa mfano:

23. (i) **A:** Bibi amenunua machungwa  
**B:** Hapana, ni [**nanasi**]<sub>F</sub> iliyonunuliwa na bibi.
- (ii) **A:** Mtoto anaendesha baiskeli  
**B:** Hapana, [**anaitengeneza**]<sub>F</sub>.  
Chanzo: Data ya Uwandani (2022)

Katika mfano wa 23 (i) na (ii), maneno yaliyokolezwa ndiyo fokasi badilishi. Viambajengo hivyo vinawakilisha taarifa mbadala kwa kuondoa taarifa ile iliyotolewa na mzungumzaji. Pia, katika mfano wa 23 (i) B, fokasi badilishi ni nomino ilhali katika 23 (ii) B fokasi badilishi ni kiarifu. Fokasi ya aina hii hung'amuliwa kwa kutumia mbinu ya usahihishaji wa taarifa. Katika mbinu hii, msikilizaji huwasilisha taarifa inayotofautiana na ile iliyotolewa na msemaji. Aidha, fokasi badilishi husimbwa kwa kutumia mikakati tofautitofauti ya kisarufi. Mathalani, katika mfano wa 23 (i) B, fokasi badilishi imesimbwa kwa kutumia mkakati wa ukasimishaji. Vilevile, katika mfano wa 23 (ii) B, fokasi badilishi imesimbwa kwa kutumia mkakati wa uwekaji wa mkazo katika tungo.

### **Hitimisho**

Makala hii imeshughulikia aina tofautitofauti za fokasi katika lugha ya Kiswahili. Uainishaji wa aina hizo umezingatia misingi anuai. Misingi hiyo ni muundo wa fokasi, mazingira ya utokeaji, dhana na lengo la mawasiliano. Aidha, fokasi zilizoainishwa huweza kung'amuliwa kwa kutumia mbinu tofautitofauti. Mbinu ambazo zimetumika kung'amua fokasi zilizoainishwa katika makala hii ni maswali na majibu, usahihishaji wa taarifa na vibainishi vya fokasi. Mbinu hizo ni miongoni mwa mbinu za ung'amuzi wa fokasi zilizopendekezwa na Van der Wal (2016). Baadhi ya mbinu za ung'amuzi wa fokasi kama vile vimanilizi, ubunifu wa kimuktadha/muktadha, na vikumushi vya nomino hazijabainika katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na hilo, tunaafikiana na watangulizi wetu kuwa usimbaji wa fokasi hutofautiana katika lugha za Kibantu na zisizo za Kibantu.

Vilevile, fokasi zilizobainika katika makala hii husimbwa kwa kutumia mikakati kadhaa ya kisarufi. Mikakati iliyobainika kusimba fokasi zilizojadiliwa katika makala hii ni ukasimishaji, utenguaji kushoto, uhamishaji wa viambajengo, unyambuaji punguzi wa vishiriki vya kitenzi na uwekaji wa mkazo katika tungo. Hata hivyo, baadhi ya mikakati tuliyoitokeza katika sehemu ya 2.3 haitumiki katika usimbaji wa fokasi katika lugha ya Kiswahili. Mathalani, uondoaji wa kiambishi tangulizi katika nomino, uhamishaji wa toni na uambishaji wa kibainishi (ne-/n) kabla ya kitenzi haitumiki katika usimbaji wa fokasi katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu utokeaji wa fokasi katika lugha ya Kiswahili huukiliwa na mpangilio wa maneno. Suala hilo ni uthibitisho tosha kuwa usimbaji wa fokasi katika lugha za Kibantu hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine.

Pamoja na hayo, dhana ya fokasi ni pana sana. Tafiti zingine zinaweza kufanyika ili kuchunguza usimbaji wa fokasi katika vipera vya fasihi simulizi kama vile nahau na hadithi katika lugha ya Kiswahili na lugha nyinginezo za Kibantu. Pia, mikakati ya usimbaji wa fokasi imedokezwa kwa kifupi katika makala hii. Kwa hiyo, utafiti wa kina unaweza kufanyika kuhusu mikakati ya usimbaji wa fokasi katika lugha ya Kiswahili na lugha nyinginezo za Kibantu.

### **Marejeleo**

- Dik, S.C. (1997a). The Theory of Functional Grammar. In K. Hengeveld (Ed.) *Part I: The Structure of the Clause*, 2<sup>nd</sup> Edition, pp. 180 - 209. Berlin, Germany: Mouton de Gruyter.
- Dik, S.C. (1997b). The Theory of Functional Grammar. In K. Hengeveld (Mh.) *Part II: Complex and Derived Constructions*, 2<sup>nd</sup> Edition, pp.117 - 136). Berlin, Germany: Mouton de Gruyter.
- Edelsten, P., Marten, L. & Lijongwa, C. (2013). Information Structure Constraint to Swahili Word Order. Makala Imewasilishwa katika Kongamano la Lugha za Kibantu Tarehe 5 Juni, 2013.
- Edenmyr, N. (2002). Focus Construction in Kirundi, (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa), The University of Stockholm.
- Hassan, F. (2019). *Uchanganuzi wa Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili*, (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Jespersen, O. (1949). *A Modern English Grammar on Historical Principals. Part VII. Syntax*. London, England: George Allen and Unwin Ltd.
- Kind, J.D. (2004). Pre-Verbal Focus in Kisikongo (H16a, Bantu). *ZAS Papers in Linguistics*, 57, 95 - 122.

- Kiss, E.K. (1998). Identificational Focus versus Information Focus. *Language*, 74 (2), 245 - 273.
- Krifka, M. (2007). Basic Notions of Information Structure. *Interdisciplinary Studies on Structure*, 6, 13 - 55.
- Lafkioui, M.B, Nshemezimana, E & Bostoan, K. (2016). Cleft Constructions and Focus in Kirundi. *Africana Linguistica*, 22, 71 - 106.
- Lambrecht, K. & Polinsky, M. (1997). Typology Variation in Sentence Focus Construction. *Panels on Linguistic Ideologies in Contact*, 33, 189 - 206.
- Landman, M. & Ranero, R. (2018). Focus Marking in Kuria. In J. Kandybowicz, T. Major, H. Torrence, na T.P. Duncan (Eds.) *African Linguistics on the Praires: Selected Paper from the 45th Annual Conference on African Linguistics*, pp 393 - 412, Berlin, Germany: Language Science Press.
- Mkude, D.J. (2005). *Passive Construction in Swahili*. Tokyo, Japan: Research Institute for Language and Culture of Asian and Africa (ILCAA).
- Mungania, B.G. & Schroeder, H. (2018). Topic, Focus and Word Order in Kiswahili Clause. *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics*, 7, 114 - 138.
- Mwamzandi, M.Y. (2014). *Swahili Word Order Choices: Insight from Information Structure* (Unpublished PhD Thesis). The University of Texas.
- Ndumiwe, E.J. (2020). *Kurunzi ya Isimu na Muundo wa Kiswahili*. Mwanza: Tridax Africa Company Limited.
- Nicolle, S. (2016). Variation in the Expression of Information Structure in Eastern Bantu Languages. In D.L. Payne, S. Pachiaroti na M. Bosire (Eds.) *Diversity in African Language*, pp. 377 - 395. Berlin: Language Science Press.

- Rooth, M. (2016). Alternative Semantics. In C. Féry and S. Ishihara (Eds.) *The Oxford Handbook of Information Structure*, pp. 260 - 288. Oxford: Oxford University Press.
- Schwarz, F. (2003). Focus Marking in Kikuyu. *ZAS Papers in Linguistics*, 30, 41 - 118.
- Van der Wal, J. (2014). Subordinate Clauses and Exclusive Focus in Makhuwa. In R.V. Gijn, J. Hammond, D. Matic, S.S. Putten and A.V. Galucio (Eds.) *Information Structure and Reference Tracking in Complex Sentences*, pp. 45 - 70. Cambridge: John Publishing Company.
- Van der Wal, J. (2016). Diagnosing Focus. *Studies in Language*, 40 (2), 259 - 301.
- Van der Wal, J. (2021). On the Use of Idioms for Testing Focus. *Semantic Field Method*, 3(3), 1 - 17.
- Van der Wal, J. na Namyalo, S. (2016). Interaction of Two Focus Marking Strategies in Luganda. In D.L. Payne, S. Pachiaroti and M. Bosire (Wah.) *Diversity in African Languages*, (355 - 377). Berlin, Germany: Language Science Press.
- Yonenda, N. (2011). Word Order in Matengo (N31): Topicality and Information Roles. *Lingua*, 121, 754 - 771.
- Zimmermann, M. (2008). Contrastive Focus and Emphasis. *Acta Linguistica Hungarica*, 55 (4), 347 - 360.